**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**

## TAARIFA KWA UMMA

### UFAFANUZI KUHUSU TAARIFA INAYOSAMBAA KATIKA MITANDAO YA KIJAMII KUHUSU VIPIMO VYA VIRUSI VYA UKIMWI VYA MARUDIO KWA AKINA MAMA WAJAWAZITO NA WANAONYONYESHA.DODOMA, 15.08.2025

Wizara ya Afya imebaini uwepo wa taarifa potofu kuhusu kupunguzwa kwa vipimo vya VVU kwa akina mama wajawazito na wanaonyonyesha kutoka vipimo vitano (5) hadi vipimo viwili (2) kuanzia kutunga mimba hadi miezi 18 ili kukinga maambukizi ya VVU kwa watoto wachanga. Taarifa hizi ni za uongo kwani vipimo hufanyika mara tatu (3) na si mara mbili (2) kama ilivyodaiwa katika taarifa hiyo ya upotoshaji.

Wizara inapenda kuujulisha umma kuwa, mwongozo wa upimaji wa VVU kwa wajawazito na wanaonyonyesha kwa lengo la kubaini maambukizi ya VVU ili kumlinda mtoto, unazingatia mapendekezo ya Shirika la Afya Duniani, matokeo ya tafiti mbalimbali, mikakati ya kitaifa na miongozo ya Shirika la Afya Duniani (WHO) na si vinginevyo .

WHO linapendekeza wajawazito na wanaonyonyesha kupima VVU mara tatu (3) au zaidi tangu kutunga mimba hadi wakati wa kunyonyesha.

Kwa muktadha huu, mikakati na miongozo ya Tanzania na kwa mujibu wa waraka wa Wizara ya Afya wa tarehe 20 Juni, 2025 unaelekeza:

- Upimaji wa kwanza wa VVU, Kaswende na Homa ya Ini unafanyika wakati wa hudhurio la kwanza la kliniki ya akina mama wajawazito na wenza wao.
- Upimaji wa pili au wa marudio unafanyika kati ya wiki ya 32 hadi wiki ya 36 za ujauzito.
- Upimaji wa tatu ni ndani ya miezi mitatu (3) baada ya kujifungua.
- Kwa wajawazito na wanaonyonyesha walio katika makundi hatarishi ya kuambukizwa VVU hupatiwa huduma ya vipimo kila baada ya miezi mitatu (3) na dawa kinga (PrEP).

Upimaji huu unatosha kubaini maambukizi ya VVU na magonjwa mengine ya ngono kwa lengo la kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Huduma hizi zinatolewa bila malipo kote nchini. Hata katika mazingira ya sasa ya kushuka kwa ufadhili wa wahisani, huduma hizo zinaendelea kutolewa kama kawaida kutokana na uwekezaji mkubwa ambao Serikali umeufanya kupitia vyanzo vya ndani.

Kwa mwaka 2024/25 Serikali ilitoa Shilingi Bilioni 141.98 na imetenga kiasi cha Shilingi Bilioni 158 kwa mwaka 2025/26 kwa ajili ya huduma za UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu, ikiwemo kuwezesha huduma za upimaji wa VVU kwa wajawazito ili kuzuia maambukizi ya VVU kwenda kwa mtoto.

Serikali inatoa wito kwa wajawazito wote kwenda kupima mara tu wanapohisi kuwa na ujauzito ili kumlinda mtoto na kutomeza maambukizi ya VVU, Kaswende na Virusi vya Homa ya Ini.

Aidha, ili kuepusha taharuki kwa umma, Wizara ya Afya inatoa wito kwa wananchi kupuuza taarifa zinazotolewa kutoka katika vyanzo visivyo sahihi na inatoa onyo kwa watu wasio na taaluma ya afya na mamlaka ya kutoa taarifa za afya kuacha mara moja kufanya hivyo. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya watakao kaidi au kuendelea kutoa taarifa za afya zisizo sahihi kwa jamii.

Imetolewa na

Dkt. Grace Magembe
**MGANGA MKUU WA SERIKALI**